OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

SHULE YA SEKONDARI MULBADAW
S. L. P 141
KATESH-HANANG
01-12-2022

Simu: **0686937744 -HM**
0755350797-HM
0682324009-S/M
Barua pepe: mulbadaw**@hanangdc.go.tz**

KUMB. NA. MSS/ADM/J.I/ K. I/VOL.1/2023

Mzazi/Mlezi wa ……

S.L.P. ……

……..

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI MULBADAW, WILAYA HANANG -2023**

Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao ……. amechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika shule ya Sekondari MULBADAW mwaka **2023. S**hule hii ni ya Daharia na kutwa, na ni mchanganyiko.

Shule hii ipo katika Wilaya ya **HANANG**, Mkoa wa **MANYARA**, Kilomita 33 Magharibi mwa mji wa **KATESH**. Aidha, Shule ipo katika kata ya MULBADAW, Tarafa ya BASOTU.
Kwa wale wanaotoka nje ya Wilaya ya Hanang, usafiri unapatikana katika kituo cha Mabasi cha **KATESH**, nauli ni Tsh 3,000/= hadi Mulbadaw Sekondari **(**CMSC**).**

Muhula wa kwanza wa Masomo utaanza tarehe 09 **Januari 2023.** Hivyo Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **09 Januari 2023** kuanzia **saa 7:30** asubuhi na mwisho wa kuripoti shuleni itakuwa tarehe **25 Januari 2023.** Ni muhimu mwanao kuripoti tarehe hiyo ili ashiriki kikamilifu katika utaratibu ulioandaliwa na shule.

Ni matumaini yangu kuwa Mwanao atatumia vizuri nafasi hii na kwamba atatumia **JUHUDI** na **MAARIFA** ya hali ya juu ili uweze kufanikiwa katika masomo na shughuli nyingine muhimu kama vile uzalishaji mali, usafi na michezo kwa kipindi chote cha uanafunzi wake hapa shuleni.

NB. *MZAZI AU MLEZI ASIACHE KUMLETA MTOTO SHULENI KWA KISINGIZIO CHOCHOTE NA IKIBAINIKA, HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YAKE*

Nakutakia maandalizi mema na karibu sana MULBADAW Sekondari.

……
SINKAMBA CM
MKUU WA SHULE

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.0 SARE ZA SHULE

wasichana

1. Shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi
2. Sketi 2 rangi ya kijani (marinda madogo ya kawaida) na kwa waislamu jalabibi/ushungi unaingia mabegani.
3. Jozi mbili za viatu vyeusi visivyo na visigino virefu, vya kufunga na kamba.
4. Jozi mbili za soksi nyeupe.
5. Sweta ya rangi ya kijani yenye shingo ya “V” isiyopasuliwa mbele
6. T- shirt ya shule, utaratibu utatolewa mara baada ya wanafunzi kuripoti
7. Raba jozi moja na nguo za michezo yaani trak suit dark blue, t-shirt ya bluu

Wavulana

1. Suruali 2 za damu ya mzee
2. Shati 2 nyeupe za mikono mifupi
3. Jozi mbili za viatu vyeusi vya kufunga na kamba, visiwe buti wala plastiki.
4. Jozi mbili za soksi ya khaki
5. Sweta ya rangi ya damu ya mzee yenye shingo ya “V” isiyopasuliwa mbele
6. T- shirt ya shule, utaratibu utatolewa mara baada ya wanafunzi kuripoti
7. Raba jozi moja na nguo za michezo yaani bukta nyekundu, t- shirt bluu.

NB: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo ambazo siyo sare ya shule. Ukaguzi utafanyika mwanafunzi anaporipoti shuleni. Kila mzazi/mlezi atawajibika kumshonea mwanaye sare hizi kabla ya kuripoti.

3.0 MAHITAJI YA CHAKULA, TAALUMA NA MAZINGIRA

A. CHAKULA

Shule hii ni ya daharia na kutwa hivyo wazazi/walezi wameweka michango ya chakula hicho kwa kila mwanafunzi kama ifuatvyo:-

(i) Mahindi debe 4 kwa muhula kwa daharia na debe moja na nusu kwa kutwa,

(ii) Maharage debe 2 kwa muhula na nusu debe kwa kutwa.

(iv) Mchango wa chakula Tsh 91,000/= kwa daharia kwa muhula na 24,500 kwa kutwa (fedha hizi zitatumika kununua, mafuta ya kupikia, sukari, chumvi, nyanya, vitunguu na posho za wapishi)

(v) Vyombo vya chakula kama vile kikombe cha uji, sahani na kijiko

Fedha zote zilipwe kupitia **A/C N0. 41010006319-CHAKULA MULBADAW SEKONDARI**

Kwa mzazi atakaehitaji mwanae kukaa Daharia awasiliane na uongozi wa shule kwanza ili kujua kama kuna nafasi. Aidha hairuhusiwi kulipa fedha taslimu kwa mtu yoyote badala yake fedha zote zipelekwe Benk kama ilivyoelekezwa.

B. TAALUMA

Kila mzazi/mlezi anawajibika kumnunulia mwanae vifaa vingine vya taaluma kama ifuatavyo:-

(i) Daftari kubwa tisa (09) countbook quire 2 au 3
(ii) Daftari ndogo za kawaida za kutosha kwa ajili ya mazoezi ya darasani
(iii) Kalamu za kutosha
(iv) Penseli kwa ajili ya michoro
(V) Rimu moja kwa ajili ya majaribio na mitihani ili kuepuka kuchana madaftari
(V) Mkebe wa hesabu, ufutio, rula n.k.
(vi) Begi zuri la kubebea madaftari na vifaa vyake vingine

C**. MAZINGIRA NA SHUGHULI ZA SHAMBA DARASA**

Moja ya mambo ambayo tunayazingatia sana hapa shuleni ni pamoja na utunzaji wa mazingira hivyo kila mwanafunzi anapokuwa shuleni atatakiwa kuwa na bustani ya maua na miti ya kutunza, ili kuifanya shughuli hii kikamilifu kila mwanafunzi anatakiwa kuleta vifaa vifuatavyo:-

(i) Ndoo safi ya lita kumi (10) kwa ajili ya kuchotea maji
(ii) Jembe lenye mpini imara kwa ajili ya kupalilia maua na miti.
(iii) Fagio moja aina ya chelewa
(iv) fagio laini moja ya dukani (soft brooms)

_____

SINKAMBA CM
MKUU WA SHULE

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE MULBADAW SEKONDARI

1. Wanafunzi wanatakiwa kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anae wazidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mkutano
2. Wanafunzi wanatakiwa kuhudhuria katika kila shughuli ndani na nje ya shule watakazopangiwa.
3. Wanafunzi wanatakiwa kujisomea kwa bidii wakati wa maandalizi ya jioni (preparation).
4. Wanafunzi wanatakiwa kuzingatia kwa makini ratiba ya shule wakati wote
5. Wanafunzi hawaruhusiwi kutumia lugha chafu kati yao wenyewe, kwa walimu wao, au kwa watu wengine wowote.
6. Wanafunzi lazima wawaheshimu wafanya kazi wasio walimu kama walezi wao.
7. Wanafunzi wanatakiwa kuwapokea walimu, wageni au wazazi mzigo mara wanapowaona wamebeba.
8. Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu na kuthamini kazi za aina zote zilizo halali.
9. Wanafunzi hawaruhusiwi kufanya mambo yafuatayo;
    a) Kuvuta sigara
    b) Kufuga kucha ndefu na kuwa na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi.
    c) Kufuga ndevu
    d) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
    e) Kugombana
10. Wanafunzi wanatakiwa kuitika mara moja, kukimbilia mahali alipo mwalimu au mtu anayewaita
11. Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, Picha za viongozi wakuu wa Inchi, Nembo ya Taifa (Court of arm), Wimbo wa Taifa na Fedha za taifa.
12. Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa chakula, ofisi za shule, mali binafsi na umma.
13. Wanafunzi wanatakiwa kusimama katika mistari wakati wa kupokea huduma kama chakula
14. Wanafunzi wanatakiwa kuwa mfano mzuri wa heshima wawapo katika mazingira ya shule na nje ya shule (mahali popote walipo)
15. Wanafunzi wanatakiwa kunyoosha mikono juu wanapouliza maswali na wasitoke darasani bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyepo.
16. Walimu, wafanyakazi wasio walimu na wanafunzi wote wanatakiwa kuheshimu na kukubali tofauti za kihali, kijinsia, kisiasa, kidini na tamaduni zilizopo katika jamii husika.
17. Mwanafuzi haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.
18. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda katika nyumba za walimu bila ruhusa ya mwalimu husika
19. Mwanafunzi anatakiwa kutoa taarifa yake ya kiafya kwa mkuu wa shule au mwalimu wa malezi bila kuficha chochote.
20. Mwanafuzi ni lazima azingatie suala la afya na kuwa msafi wakati wote, pia kuhakikisha kuwa mazingira yote ya shule ni masafi kila wakati.

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uwasherati, ubakaji, ushoga na kusagana.
3. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile; uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
4. Makosa yote ya jinai.
5. Kupiga au kupigana.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau bendera ya taifa.
8. Kuoa au kuolewa
9. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
10. Kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea, kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Kumiliki au kukutwa na simu au ‘line’ ya simu ya mkononi.

NB. KUTOJUA SHERIA SI KINGA YA KUTOADHIBIWA
NAKUTAKIA UTIIFU NA UTEKELEZAJI MWEMA WA SHERIA ZA SHULE